**SHERIA YA MAREKEBISHO YA SABA YA KATIBA YA ZANZIBAR NAM. 11 YA 1995.**

## YALIOMO:

| KIFUNGU: | MAELEZO: |
| --- | --- |
| 1. | Jina fupi na kuanza kutumika. |
| 2. | Marekebisho ya Kifungu cha 34. |
| 3. | Marekebisho ya Kifungu cha 36A. |
| 4. | Marekebisho ya Kifungu cha 39A. |
| 5. | Marekebisho ya Kifungu cha 41. |
| 6. | Marekebisho ya Kifungu cha 77. |
| 7. | Marekebisho ya Kifungu cha 85. |
| 8. | Marekebisho ya Kifungu cha 91. |
| 9. | Kuweka Kifungu Kipya cha 96A. |

*NAM. 11 YA 1995.*

***NAKUBALI***

Salmin Amour

***DK. SALMIN AMOUR***

***RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI.***

14th August 1995.

***SHERIA YA KUREKEBISHA KATIBA YA ZANZIBAR YA 1984.***

***IMETUNGWA*** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Jina fupi na kuanza kutumika

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Saba ya Katiba ya Zanzibar, 1995 na itasomwa pamoja na Katiba ya Zanzibar, 1984 na kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Marekebisho ya kifungu cha 34.

2. Kifungu cha 34 cha Katiba kinarekebishwa katika kijifungu (1) kama ifuatavyo;

"(1) Endapo kiti cha Rais kiwazi kwa sababu ya kufariki au kujiuzulu au kwa maradhi chini ya kifungu cha 33 cha Katiba hii, au kwa sababu nyengine yoyote, nafasi hiyo itajazwa kama ifuatavyo;-

(i) Iwapo Rais aliyekuwapo ametumikia kwa muda wa chini ya miaka minne basi mt u anayemfuatia kwa madaraka atachukua madaraka ya Urais kwa muda na uchaguzi utaitishwa ndani ya siku mia moja na ishirini.

(ii) Iwapo Rais aliyekuwepo ametumikia Urais kwa miaka minne au zaidi, basi mtu anayemfuatia kwa madaraka atachukua madaraka ya Urais na ataendelea na madaraka hayo kwa kipindi kilichobaki cha muda wa Urais.

(iii) Mtu atayechukua madaraka hayo ya Urais atakuwa na madaraka yote ya Rais, kwa mujibu wa Katiba, na atateua Waziri Kiongozi, Baraza la Mawaziri na Viongozi wengine kadri atavyoona inafaa."

Marekebisho ya kifungu cha 36 A.

3.(1) Kifungu cha 36A cha Katiba kinarekebishwa kwa kuondoa kijifungu (7) na kuweka badala yake kijifungu (7) kipya kama ifuatavyo;

"(7) Endapo Rais ataacha kushika kiti cha Rais kutokana na mashtaka dhidi yake kuthibitika:

(i) hatakuwa na haki ya kupata malipo yoyote ya pencheni wala kupata haki au nafuu nyenginezo alizonazo kwa mujibu wa Katiba au Sheria yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi: na

(ii) hataweza kugombea tena nafasi ya Urais au Uwakilishi kwa muda wa miaka mitano tokea siku aliyoachishwa Urais"

Isipokuwa pindi Rais huyo akiwa ameshatumikia kipindi cha miaka mitano (5) ya awali na akakutwa na mashtaka katika kipindi cha pili basi atapata nusu ya haki na nafuu nyenginezo alizonazo kwa mujibu wa Katika au Sheria yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Marekebisho ya kifungu cha 39A.

4. Kifungu cha 39 A cha Katiba kinarekebishwa kwa kuongeza kijifungu kipya cha (7) mara tu baada ya kijifungu (6) kama ifuatavyo:

"(7) Endapo Waziri Kiongozi ataacha kushika wadhifa wake huo kutokana na Azimio la hoja ya kura ya kutokuwa na imani-

(i) hatakuwa na haki ya kupata malipo yoyote ya pencheni wala kupata haki au mafuu nyenginezo, kwa mujibu wa Katiba au Sheria yoyote iliyotungwa na Baraza: na

(ii) atabaki kuwa Mwakilishi lakini hataweza kuteuliwa tena kuwa Waziri Kiongozi, Waziri, Naibu Waziri au Mkuu wa Mkoa kwa kipindi chote cha uhai wa Baraza hilo.

Marekebisho ya kifungu cha 41.

5. Kifungu cha 41 cha Katiba kinarekebishwa kwa kuondoa kijifungu (1) kiliopo na badala yake kuweka kipya kifuatacho:

"(1) Kutakuwa na Baraza la Mapinduzi ambalo litajumuisha Rais, Waziri Kiongozi, Mawaziri pamoja na Wajumbe wengine kama Rais atakavyoona inafaa."

Kufanya mabadiliko katika kifungu cha 77.

6. Kifungu cha 77 kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 77 kifuatacho:

"Afisi ya Baraza la Wawakilishi.

77(1) Kutakuwa na Afisi ya Baraza la Wawakilishi itayoongozwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi na itakuwa na nafasi za madaraka kama itavyoidhinishwa na Tume ya Utumishi wa Baraza la Wawakilishi.

(2) Kutakuwa na Tume ya Utumishi wa Baraza la Wawakilishi ambayo itakuwa na uwezo wa kuajiri maafisa na watumishi wote wa Baraza, kuwapandisha vyeo, kuwachukulia hatua za kinidhamu na kufanyakazi nyengine zozote zitazoelezwa na Sheria kuhusu Utumishi katika Afisi ya Baraza. Isipokuwa kwamba Katibu wa Baraza la Wawakilishi atateuliwa na Rais kwa mujibu wa kifungu cha 76 cha Katiba.

(3) Muundo na taratibu za Tume ya Utumishi wa Baraza utakuwa kama itavyoelezwa na Sheria itayotungwa kwa madhumuni hayo.

(4) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga Sheria ya kuweka mfumo wa utawala na uendeshaji na mambo mengine yanayohusu Afisi ya Baraza la Wawakilishi.

Kufanya mabadiliko katika kifungu cha 85.

7. Kifungu cha 85 kinarekebishwa kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kukiondoa kijifungu (1) na kuweka badala yake kijifungu kipya kifuatacho

"(1) Kutakuwa na Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zitazoundwa kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

(b) Kijifungu (3) kinarekebishwa kwa kuondoa neno "nyengine" mara baada ya neno "Kamati".

Marekebisho ya kifungu cha 91.

8.(1) Kifungu cha 91 kinafanyiwa marekebisho kwa kukifuta kijifungu (2) na kuweka badala yake kijifungu kipya (2) kifuatacho:-

"(2) Rais hatakuwa na uwezo wakati wowote wa kilivunja Baraza la Wawakilishi isipokuwa tu:

(a) Kama Baraza la Wawakilishi limemaliza uhai wake kwa mujibu wa kifungu cha 92 cha Katiba;

(b) Anaweza kulivunja wakati wowote ndani ya miezi kumi na mbili ya mwisho ya uhai wa Baraza la Wawakilishi kwa madhumuni ya kuitisha Uchaguzi mapema kidogo.

(c) Kama Baraza la Wawakilishi limekataa kupitisha Bajeti inayopendekezwa na Serikali

(d) Kama Baraza la Wawakilishi limekataa kupitisha Mswaada wa Sheria kwa mujibu wa kifungu cha 79 cha Katiba;

(e) Kama Baraza la Wawakilishi limekataa kupitisha hoja ambayo ni ya msingi katika sera za Serikali na Rais anaona kwamba njia muafaka ya kulinda maslahi ya Taifa si kuvunja Baraza la Mawaziri au kuteua Waziri Kiongozi mpya bali ni kuitisha Uchaguzi Mkuu;

(f) Endapo, kutokana na uwiano wa uwakilishi wa Vyama vya Siasa katika Baraza la Wawakilishi, Rais anahisi kwamba hakuna uhalali kwa Serikali iliyopo kuendelea kuwapo na wala haiwezekani kuunda Serikali mpya.

Isipokuwa kwamba hataweza kulivunja Baraza chini ya masharti ya ibara (b) (c) (d) (e) na (f) kama Spika amepokea taarifa rasmi inayopendekeza kuundwa kwa Kamati Maalum ya Uchunguzi kwa madhumuni ya kumuondoa Rais madarakani kwa mujibu wa kifungu cha 36A cha Katiba;

(2) Kwa kuweka kijifungu (3) kifuatacho:-

"(3) Bila ya kuathiri masharti yoyote ya Katiba, Spika anaweza wakati wowote kuliitisha Baraza la Wawakilishi kwa jambo la dharura baada ya kupata ombi la Mjumbe wa Baraza la Wawakilshi linaloungwa mkono na nusu ya Wajumbe wote wa Baraza na Spika akaridhika kwamba sababu zilizoelezwa katika ombi hilo ni za msingi na inafaa Baraza la Wawakilishi kuitishwa".

Kuweka kifungu kipya cha 96A.

9. Katiba inafanyiwa marekebisho kwa kuongeza baada ya kifungu cha 96 cha Katiba kifungu kipya kifuatacho:-

"Uanachama katika Vyama vya Siasa.

96A. Itakuwa ni marufuku kwa Jaji wa Mahkama Kuu (pamoja na Jaji Mkuu), Mahakimu wa ngazi zote, Mrajis, Kaimu Mraji, Naibu Mrajis na Msaidizi Mrajis na Makadhi wote (pamoja na Kadhi Mkuu) kujiunga na Chama chochote cha Siasa isipokuwa tu kwamba atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika kifungu cha 7 cha Katiba hii".

***Imepitishwa*** katika Baraza la Wawakilishi tarehe 17 Julai, 1995.

K.J. Chande

***(KHAMIS JUMA CHANDE)***
***KATIBU***
***BARAZA LA WAWAKILISHI.***